



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA



Tovuti: www.hlpc.go.tz

TANGAZO

KUPATIWA AKAUNTI ZA KUINGIA KWENYE MFUMO WA USAJILI (HPRS)

Baraza la Wataalam wa Maabara linaendelea na zoezi la kupokea taarifa za kuwatengenezea akaunti Wataalam ambao bado hawajaingizwa kwenye mfumo;

1. Zoezi hili linawahusu Wataalam wote ambao hawana akaunti kwenye mfumo wa HPRS. Kwa Mtaalam ambaye tayari ana akaunti kwenye mfumo wa HPRS (hprs.moh.go.tz) hatakiwi kutuma tena taarifa zake.
2. Wataalam ambao walisajiliwa kwa usajili wa kudumu (Enrollment / Full) kabla ya mfumo kuanza na bado hawajatumiwa taarifa za kuingia kwenye mfumo ndio wanatakiwa kuwasiliana na ofisi kwa ajili ya kutoa taarifa zao
3. Wataalam wote wanaotumiwa ujumbe mfupi wa meseji (SMS) wenye taarifa za kuingia kwenye mfumo **hawatatakiwa ku create account**. Wanatakiwa ku-login kwa Email na Password wanazotumiwa.
4. Mawasiliano ya ofisi yafanyike ndani ya muda wa kazi wa Serikali kuanzia saa mbili kamili asubuh hadi saa tisa na nusu alasiri kwa siku ya Jumatatu hadi Ijumaa.
5. Kwa msaada wa karibu jinsi ya kuingia kwenye mfumo tuwasiliane na Waratibu wa huduma za Maabara Mikoa na Wilaya watatusaidia ikiwemo kutupatia miongozo (System User Manual)

Ofisi ya Msajili inawasisitiza Wataalam wote kuzingatia maelekezo.

Maneno laofisi: Simu: 0734005777, Email: hlpc@afya.go.tz

Imetolewa na:

Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara.

